TOLEO MAALUMU Na. 171 | SEPTEMBA 2024

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

JARIDA LA

# JIJI LETU



MKURUGENZI WA JIJI DSM AKAGUA MIRADI YA ZAIDI YA BILIONI 5 INAYOTEKELEZWA ...Uk 4

MHE.MCHENGERWA: SITOSITA KUMCHUKULIA HATUA ATAKAEJIUSISHA NA UBADHIRIFU WA MIKOPO YA ASILIMIA 10 ...Uk 2

## RAIS SAMIA AWAKUMBUKA WANANCHI KIPUNGUNI ...UK 1

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024 – JIANDIKISHE PIGA KURA – OFISI YA RAIS TAMISEMI

JIANDAE KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA NOVEMBA 27, 2024.




# RAIS SAMIA AWAKUMBUKA WANANCHI WA KIPUNGUNI

**Na** Mariam Muhando

Mkuu wa Wilaya ya Ilala mheshimiwa Edward Mpogolo, amesema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo kuwa wananchi waliopisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) kulipwa fidia zao.

Mhe. Mpogolo ameyasema hayo wakati akiwa katika mkutano wa hadhara wa kusikiliza na kutatua kero za wanchi wa Kata za Minazi mirefu, Kiwalani na Kipawa.
Aidha amezitaka kamati za wananchi wa mtaa wa Kipunguni kata ya Kipawa Ilala, jijini Dar es Salaam, kufika ofisini kwake ili kupewa maelekezo Zaidi kuhusu zoezi hilo.

"Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, ameshatoa maelekezo kwamba malipo yaanze kufanyika ambapo kwa sasa kinachosubiliwa ni mifumo wa namna ipi malipo hayo yafanyike".Alisema Mpogolo.

Baadhi ya wananchi walioongea na mwandishi wa Habari hii walimshukuru mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kumaliza Sakata hilo lililochukua muda mrefu.

"Kwa kweli tulishachoshwa na danadana za kulipwa fidia zetu kwa kipindi kirefu ila kwa sasa tuna uhakika wa kupata haki zetu na tunasubiri wawakilishi wetu waende ofisini kwa mkuu wa Wilaya kwa ajili ya mchakato wa malipo" Alisema mmoja wa wananchi katika mkutano huo.

Mgogoro huo kuhusiana na malipo ya fidia kwa ajili ya kupisha upanuzi wa Uwanja huo wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere yamekuwa ya muda mrefu kwa wakazi hao ambao kwa sasa wamepata Faraja mpya kufuatia kauli hiyo ya Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.





# MHE.MCHENGERWA: SITOSITA KUMCHUKULIA HATUA ATAKAEJIUSISHA NA UBADHIRIFU WA MIKOPO YA ASILIMIA 10

**Na** James K. Mwanamyoto OR-TAMISEMI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa amesema hatosita kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria maafisa maendeleo ya jamii, wasimamizi wa fedha, waratibu wa mikopo, wahasibu na maafisa TEHAMA wa Mikoa na Wilayq ambao watabainika kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za mikopo ya asilimia 10 zinazotolewa na Halmashauri kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wanye ulemavu.

Waziri Mchengerwa ameyasema hayo leo Jijini Dodoma katika ukumbi wa Chuo cha Mipango, wakati akifunga mafunzo ya wasimamizi wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambayo inatokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini.

"Mikopo hii inatolewa na Serikali kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kujikomboa kiuchumi kwa kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali, hivyo sitosita kuwachukulia hatua watakaokwamisha makundi lengwa kupata mikopo," Mhe Mchengerwa amesisitiza.

Mhe. Mchengerwa amesema mikopo hii ikisimamiwa vizuri na kuwafikia walengwa itabadilisha maisha ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hivyo amewataka washiriki wa mafunzo hayo waende kutoa elimu ya namna bora ya kuitumia mikopo hiyo kuboresha maisha yao ili waweze kufanya marejesho kwa wakati na kuwezesha wengine kunufaika.

Waziri Mchengerwa amewataka wasimamizi wa mikopo ya asilimia 10 kuratibu utoaji wa mikopo hiyo kwa uzalendo ili iwanufaishe walengwa na iwe na tija kwa jamii na maendeleo ya taifa kwa ujumla kama ilivyo kusudiwa na Serikali.

Mpaka kufika mwaka wa fedha 2024/25 fedha ambazo zimetengwa kutoka kwenye marejesho ya mikopo ya nyuma pamoja na mapato ya ndani ya Halmashauri tangu utoaji wa mikopo hii ulipositoshwa ni zaidi ya shilingi bilioni 160 kwa Halmashauri zote nchini na fedha hizi zitatumika kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, pamoja na usimamizi wa mikopo hiyo.

Ikumbukwe kuwa mikopo hii inatokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini.




# MKUU WA MKOA WA DSM AZINDUA KONGAMANO LA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Na** Mariam Muhando

Katika kuhakikisha mkakati wa miaka 10 wa matumizi ya nishati safi ya kupikia unatekelezwa kwa ufanisi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila amezindua kongamano la matumizi ya Nishati safi ya kupikia katika viwanja vya Karimjee Jijini Dar es salaam.

Kongamano hilo lilifanyika mnamo Septemba 12,2024 na kuhudhuriwa na Wakuu wa Wilaya, Mameya, Wakurugenzi wa Halmashauri,Watendaji Wakuu wa Taasisi ambata za Nishati safi, Viongozi wa dini na mamia ya mama lishe na baba lishe.

Akizindua kongamano hilo RC Chalamila ameishukuru kampuni ya Lake Gas kwa kutoa mitungi 1000 ya Nishati safi kwa kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan katika kuachana na matumizi ya Nishati chafu badala yake kutumia Nishati safi ya kupikia.

"Niwaombe Taasisi, Mashirika na wadau wengine ndani ya Mkoa huu kuiga mfano wa kampuni ya Lake Gas kuendelea kutoa mitungi zaidi ya gesi ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi." Alisema RC Chalamila.

Sambamba na hilo RC Chalamila amemuagiza Katibu Tawala wa Mkoa kuratibu upatikanaji wa mitungi ya gesi kutoka Taasisi mbalimbali za serikali kuchangia mitungi kuanzia 200 hadi 300 kabla ya Septemba 30/2024 huku akisisitiza kuwa kampeni ya matumizi ya nishati safi ni endelevu na lengo ni kuwafikia wananchi wengi zaidi.

> SERIKALI INALENGA KUONGEZA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUFIKIA 80% YA WATANZANIA WANAOTUMIA NISHATI HIYO.

Ikumbukwe kuwa mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan Mei 8, 2024 ukilenga kuepuka athari za matumizi ya kuni na mkaa.





# MKURUGENZI WA JIJI DSM AKAGUA MIRADI YA ZAIDI YA BILIONI 5 INAYOTEKELEZWA KATIKA JIJI HILI

**Na** Judith Damas

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam ndugu Elihuruma Mabelya ametembelea na kukagua miradi minne ya elimu na Afya yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 5 inayotekelezwa na Jiji hili ikiwa kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

Katika ziara hiyo Mkurugenzi Mabelya aliweza kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Mzinga chenye thamani ya shilingi bilioni 2 fedha kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri, mradi ukiwa umekamilika kwa asilimia 65% ujenzi wa madara 20 ya ghorofa na matundu 45 ya vyoo shule ya Sekondari Kipunguni yenye thamani ya shilingi bilioni 1.3.

Aidha alitembelea ujenzi wa madarasa 20 ya ghorofa na matundu 45 ya vyoo shule Mpya ya Sekondari Amani yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 fedha zilizotokana na na mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo mradi huo unatarajiwa kukamilika Octoba 2024 pamoja na ujenzi wa madara 20 ya ghorofa na matundu 45 ya vyoo Shule ya Sekondari Mnazi Mirefu yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 fedha kutoka Serikali kuu na mapato ya ndani ya Halmashauri, mradi ukiwa kwenye hatua za umaliziaji sakafu ya tano.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi huyo amewashukuru na kuwapongeza wataalamu wa Jiji la Dar es Salaam kwa kuendelea kusimamia na kufuatilia miradi hiyo kwa ukaribu zaidi huku akiwaagiza wataalamu hao kuhakikisha wanasitisha mkataba kwa mkandarasi atakayekiuka masharti ya mkataba pamoja na kuhakikisha wakandarasi wanao watumia wana uwezo zaidi lengo likiwa ni miradi kukamilika kwa wakati.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Mwl. Mussa Ally amemshukuru Mkurugenzi wa Jiji kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati huku akimuahidi kusimamia kwa ukaribu miradi hiyo pamoja kumpa ushirikiano kwa kutekeleza yote aliyowaelekeza kwa maendeleo ya Jiji na Taifa kwa ujumla.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

JIANDIKISHE PIGA KURA

2024

OFISI YA RAIS TAMISEMI

**EWE MWANANCHI, JIANDAE KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA NOVEMBA 27, 2024.**



# MAKALLA ARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO JIJI LA DSM

**Na** Mariam Muhando

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, CPA Amos Makalla, ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

CPA Makalla amebainisha hayo alipokuwa katika ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika Jimbo la Segerea ambapo alitembelea mradi wa ujenzi wa madarasa 20 Shule ya Sekondari Minazi mirefu wenye thamani ya shilingi bilioni 1.79 pamoja na Mradi wa Kituo cha Afya Kinyerezi chenye thamani ya shilingi milioni 500

”Niwapongeze Mkuu wa wilaya ya Ilala kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Jiji kwa utekelezaji huu wa Miradi kwa kuwa nia ya Serikali ni kuboresha huduma kwa wananchi na kubwa zaidi mmeweza kutekeleza miradi hii kwa kutumia fedha za mapato ya ndani na nyingine za Serikali kuu hizi ni jitihada nzuri mnazozifanya za kuendelea kuboresha huduma za afya na Elimu kwa Wananchi wa Jiji la Dar es Salaam”.Alisema Katibu huyo wa Itikadi,Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa

Kwa upande wake mkuu wa wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha huduma za elimu na afya katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutoa fedha nyingi z kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu lengo likiwa ni kuhakikisha sekta hizo zinakua imara na wananchi wanapata huduma bora na kwa wakati.

Serikali imeendelea kuwekeza katika sekta ya elimu na Afya katika Jiji la Dar es Salaam ambapo shule za ghorofa zaidi ya 8 zinaendelea kujengwa zikiwa katika hatua mbalimbali hali ambayo itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na kuongeza ufaulu zaidi.



# MKURUGENZI MABELYA AHIMIZA WAKANDARASI KUKAMILISHA MIRADI KWA WAKATI

**Na** Judith Damas

Wakandarasi wanaotekeleza Miradi mbalimbali ya maendeleo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wametakiwa kufanya kazi kwa uadilifu na kukamilisha miradi kwa wakati kwa kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa viwango na ufanisi unaotakiwa ili kuendana na thamani ya fedha.
Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam ndugu Elihuruma Mabelya wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Jiji hili.

Mkurugenzi Mabelya Ameeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ina lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa wakati hivyo kutoa wito kwa wakandarasi wote kuhakikisha wanakamilisha miradi kwa wakati huku akiwataka wataalamu kutoka Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha wanafuatilia miradi hiyo kwa ukaribu zaidi.

“Nimetembelea na kukagua miradi minne ya Afya na elimu lakini pia kubaini changamoto za miradi hiyo na kuweza kuzitatua ili kazi iendelee kwani kupitia miradi hii tunaamini wananchi wetu wataendelea kupata huduma stahiki kwa wakati hivyo niwaagize wakandarasi wote ambao wamesimama kuendelea na utekelezaji kwa sababu mbalimbali warudi kazini kuanza utekelezaji ili miradi hiyo iweze kukamilika kwa wakat’.Alisema Mabelya.

Sambamba na hilo Ndg. Mabelya amewasisitiza Wakandarasi hao kushirikiana na wataalamu kutoka ofisi yake pindi wanapokutana na changamoto zozote wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo lengo likiwa ni kutatua changamoto hizo.

Akiongea kwa niaba ya Mkandarasi Humphrey Constraction ambaye anatekeleza mradi wa Kituo cha Afya Mchikichinii Mhandisi amemuhakikishia Mkurugenzi wa Jiji la Dar ea Salaam kuwa ujenzi huo unatarajiwa kuendelea haraka iwezekanavyo ili ukamilike kwa wakati.

Miradi iliyotembelewa ni pamoja na Ujenzi wa Kituo cha Afya Mchikichini, ujenzi wa Maktaba na Ukumbi Shule ya Sekondari Benjamini Mkapa, Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa nyasi bandia Shule ya Sekondari Benjamini Mkapa pamoja na kukagua maendeleo ya mradi wa Machinjio ya Vingunguti ambapo miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.




# JIJI LAPANGA KUKUSANYA ZAIDI YA MILIONI 973 KUTOKANA NA KODI ZA NYUMBA ZA KULALA WAGENI



**Na** Mariam Muhando

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imepanga kukusanya Kodi ya Nyumba za kulala Wageni "Hoteli Levy" zaidi ya Shilingi Milioni 973 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/ 2025.

Hayo yamebainishwa na Meneja wa Kodi ya Nyumba za kulala Wageni kutoka halmashauri ya Jiji la Dar es salaam Bi.Karoline Latemba Septemba 21,2024 katika mafunzo yaliowakutanisha Watumishi mbalimbali kwenye Ukumbi wa Anatoglo Jijini humo kwa lengo la kuwajengea uwezo wa ukusanyaji kodi na kuzipatia Ufumbuzi changamoto wanazokabiliana nazo ambapo amesema kulingana na bajeti hiyo,Jiji limeamua kuwajengea uwezo Watumishi hao.

Latemba amesema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo Wafanyabiashara ambao hawana utayari wa kulipa Kodi,hivyo Mafunzo hayo yatawasaidia kutatua changamoto hiyo.

"Ili kuzipatia Ufumbuzi changamoto tunahakikisha tunakuwa na ukaribu na Wafanyabiashara hivyo tutatumia Sheria za Kodi hiyo ikiwemo kufanya ukaguzi ili kuona vitabu vya wageni katika hotel zao vinajazwa ipasavyo sambamba na kutoa elimu ya ulipaji kodi."Amesema Latemba.

Katika hatua nyingine amewataka Wafanyabiashara Jijini humo kuhakikisha wanalipa Kodi ili kuiwezesha Serikali katika kuleta huduma mbalimba katika Jamii.

Nao baadhi ya Watumishi walioshiriki Mafunzo hayo wamemshukuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ndugu Elihuruma Mabelya Kwa kuwaandalia Mafunzo hayo ambayo yatakayowawezesha kuwajengea uwezo wa Ukusanyaji wa Mapato na kufanya kazi Kwa weledi ili kufikia lengo la Jiji hilo.

Ikumbukwe kuwa katika kipindi Cha Mwaka wa fedha 2024 hadi 2025 Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam inatarajia kukusanya Zaidi ya Shilingi Bilioni 130 ili kuiwezesha Serikali katika kuwaletea Wananchi huduma mbalimbali za maendeleo Jijini humo.



# JIJI LA DSM LIMEKUWA MFANO WA KUIGWA KATIKA SEKTA YA ELIMU

**Na** Mariam Muhando

Viongozi mbalimbali kutoka Visiwani Zanzibar mapema mwezi huu walifanya ziara ya mafunzo katika halmashauri ya Jiji la Dar es salaam kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu katika eneo la Sekta ya Elimu.

Viongozi hao wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Elimu Mjumuisho Zanzibar Bw.Juma Alli wameweza kujifunza mambo mbalimbali ambayo Jiji la Dar es Salaam inayafanya ikiwemo zoezi la upimaji satoto kabla ya kuanza shule ili kubaini changamoto wanazokabiliana nazo.

Akizungumza mara baada ya kupokea Viongozi hao Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam ndugu Elihuruma Mabelya ameeleza kuwa ujumbe huu unaonesha jinsi gani Jiji la Dar es Salaam limejiimarisha katika eneo la Sekta ya Elimu na kuwa kivutio kwa wengine kuja kujifunza.



Aidha Mkurugenzi Mabelya amemshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muumgano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha anazoendelea kuzileta katika halmashauri ya Jiji la Dar es salaam zinazosaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya Elimu.

Nae Mkuu wa kitengo Cha Elimu Mjumuisho Zanzibar kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya amali Bw. Juma Alli amesema wamejifunza mengi kupitia ziara hiyo na wataenda kuyafanyia kazi yale yote waliyojifunza.

Kutokana na changamoto zilizokuwa zikijitokeza mashuleni,Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam limeamua kuzipatia ufumbuzi kwa kuwapima Watoto hao ili kugundua changamoto mbalimbali zinazowakabili kabla ya kujiunga na elimu ya msingi.

CITY FM RADIO
91.7 Mhz

# SIKILIZA 91.7 FM DSM

Redio inayomilikiwa na kuendeshwa chini ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini(GCU) - Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.





**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
S.L.P 20950
1 BARABARA YA MOROGORO
11882 DAR ES SALAAM
**SIMU:** 0738 378 386
**NUKUSHI:** 2128800
**BARUA PEPE:** info@dcc.go.tz
**TOVUTI:** www.dcc.ho.tz

**JIANDAE KUSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA NOVEMBA 27, 2024.**